

NATIONAL INVESTMENTS PLC



TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 7 WA WANAHISA WA NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL)

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 7 wa mwaka wa Wanahisa wa NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL) utafanyika katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) siku ya Ijumaa, tarehe 3 Desemba, 2021. Kuanzia saa 4:00 asubuhi. Dawati la usajili litafunguliwa mapema kuanzia saa mbili na nusu asubuhi (2:30 asubuhi).

Ajenda ya Mkutano ni kama ifuatavyo:

- 7.1. MATANGAZO NA AKIDI
- 7.2. KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
- 7.3. KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 6 ULIOFANYIKA TAREHE 21 NOVEMBA 2020.
- 7.4. YATOKANAYO NA MKUTANO WA 6 WA WANAHISA
- 7.5. KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2020.
- 7.6. MAPENDEKEZO/TAMKO LA GAWIO KWA MWAKA WA FEDHA UTAKAOISHIA 2021.
- 7.7. KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI.
- 7.8. KUJIUZURU NA KUTEULIWA KWA WAKURUGENZI
- 7.9. KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2021.
- 7.10. MENGINEYO.

MAELEZO MUHIMU:

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano ni lazima kuwasilisha nyaraka zifuatazo: nakala ya stakabadhi yake ya Hisa (Depository Receipt) pamoja na Kitambulisho cha Kitaifa au kitambulisho cha mpiga kura, pasipoti (pasi ya kusafilia) au leseni ya udereva.
2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi za NICOL zilizopo Mtaa wa Mirambo, Mirambo House, Gorofa ya Tatu (au kwa njia ya barua pepe invest@nicol.co.tz) kabla ya saa 10 Alhamisi ya tarehe 2 Desemba 2021.
3. Nakara za Taarifa ya Mwaka na fomu za uwakilishi (Proxy forms) zinapatikana katika ofisi za NICOL au unaweza kuzipakua katika tovuti ya NICOL's (www.nicolplc.co.tz). Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kwa simu Na. 0733 006 177 au 022 2111 399.

Kwa Idhini ya Bodi

Adv. Benjamin Mwakagamba
Katibu wa Kampuni